

SHULE YA SEKONDARI SHIRATI SOTA
S.L.P. 59.
SHIRATI RORYA.
TAREHE. 14.12.2020

KUMB NA: SHRT SOTA. SS/VOL. 01/2020

JINA LA MWANAFUNZI.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SHIRATI SOTA,
WILAYA YA RORYA, MKOA WA MARA MWAKA 2021

1.0 UTANGULIZI.

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza (I) mwaka katika shule ya Sekondari Shirati sota. Shule hii ipo umbali wa Km 25 Kusini mwa Halmashauri ya Wilaya ya Rorya.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe.....Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe mwisho wa kuripoti ni tarehendani ya siku saba tu. Vinginevyo iwe kwa ruhusa maalumu ya mkuu wa shule tu.

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

(a) Sare za shule

- Mashati mawili(2) meupe ya mikono mifupi.
- Suruali mbili (2), moja rangi nyeusi na ya pili rangi ya kijani jani la mgomba kwa wavulana, yenye malinda mawili na isiyokuwa mtindo wa modo. Suruali lazima zivaliwe na mikanda ya rangi nyeusi.
- Sketi mbili (2), moja rangi nyeusi, ya pili rangi ya kijani jani la mgomba kwa wasichana, ndefu zenye kufunika magoti na zinazokaribia kugusa visigino. Sketi ziwé na malinda 8 au yasiyozidi 19. Kitambaa kiwe kizito na sio tetron, Sketi fupi na vimini ni marufuku.
- Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba ila visiwe mtindo wa buti. Raba, simple, viatu vya mpira kama mabondo na kandambili haziruhusiwi kwa wavulana na wasichana.
- Soksi ndefu nyeupe kwa wasichana na nyeusi kwa wavulana.
- Sweta mbili (i) rangi ya kijani jani la mgomba na (ii) sweta rangi nyeusi kwa wavulana na wasichana.

(b) Sare na vifaa vya michezo.

- Raba
- T-shirt nyeusi yenye kofa nyeupe
- Bukta ya bluu kwa wavulana na traki sutiya bluu kwa wasichana.

3.0 MAMBO MENGINE

- Kalamu, madaftari 9 (countre books quire 2)
- Madaftari 9 kwa ajiri ya mazoezi ya darasani
- Mkebe wa hisabati (mathematical set)
- Kamusi ya kiingereza kwa kingereza yaani ADVANCED LEARNERS OXFORD DICTIONARY
- Ream paper moja ya A4
- Fedha ya walimu masomo ya sayansi miezi mitatu Shilingi elfu tisa tu (Tshs 9000/=)
- Kila mwanafunzi afike siku ya kuripoti shuleni akiwa na kiti cha mbao na meza ya mbao ya kusomea darasani.

4.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1975 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi yenye dhamana ya kutoa elimu nchini na ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
3. Kuwahi katika kila shughuli ya shule na nyingine utakazopewa.
4. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule.
5. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
6. Kuvaa sare ya shule wakati wote ukiwa shuleni siku za shule.
7. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

8. Kutunza mali za umma.

4.2. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

1. Wizi
2. Uasherati na Ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli, uvutaji wa sigara n.k
5. Kupigana ua kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau bendera ya Taifa
8. Kuwa mjamzito, kupata mimba, au kusababisha mimba
9. Kugoma au kuchochea na kuongoza mgomo au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
10. Kuoja au kuolewa
11. Kukataa kufanya adhabu
12. Kuwa na simu ya mkononi shuleni

4.3 MAELEZO MUHIMU.

Ni muhimu kwa mzazi/mlezi wa mwanafunzi kusoma na kuelewa vema sheria na kanuni za shule kisha kujaza fomu hii na kuikabidhi siku ambayo mwanafunzi ataripoti shuleni. Unatakiwa kumleta mwanao shuleni, wewe mwenyewe, siku ya kufungua shule tarehe..... akiwa ametimiza mahitaji yote ya shule, bila kukosa.

SEHEMU YA MWANAFUNZI

Mimi(jina kamili, majina matatu) ambaye nimechaguliwa kujiunga na masomo kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Shirati Sota kwa mwaka wa masomo..... ninaahidi kuwa nimesoma na kuelewa kanuni na sheria za shule na nimekubali kufuata sheria na kanuni hizo zote.

JINA (mwanafunzi)

Sahihi.....

SEHEMU YA MZAZI

Mimi (mzazi/mlezi) wa..... (jina la mwanafunzi), ninaahidi kumlea mwanangu kulingana na sheria na kanuni za shule. Mwanangu amekubali kufuata sheria na kanuni za shule. Pia ninaahidi kushirikiana na walimu kumlea kwa mujibu wa sheria na kanuni za shule.

JINA (mzazi/mlezi).....

SAHIHI.....



THE HEADMASTER
SHIRATI SOTA SEC. SCHOOL
BOX 250
RORYA

KAPEYA BUTU

MKUU WA SHULE

SHIRATI SOTA SEKONDARI